TANGAZO LA SERIKALI Na. 228 la tarehe 5/4/2024

SHERIA YA TAASISI YA UTAFITI WA MIFUGO TANZANIA
SURA YA 434

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 6(4))*

AMRI YA KUANZISHA KITUO CHA UTAFITI WA MIFUGO CHA NSIMBO YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kuanzisha Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Nsimbo ya Mwaka 2024.

Kuanzishwa kwa Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Nsimbo

2. Kinaanzishwa kituo cha utafiti wa mifugo kitakachojulikana kama "Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Nsimbo" ambacho kitahudumia kwa Mikoa ya Kigoma, Tabora naa Katavi.

Majukumu ya Kituo
Sura ya 434

3. Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Nsimbo kitatekeleza majukumu yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria ya Utafiti wa Mifugo na kitakuwa chini ya udhibiti na usimamizi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania.

Dodoma
……….....…, 2024

ABDALLAH HAMIS ULEGA,
*Waziri wa Mifugo na Uvuvi*